

102/1

2020 FORM 4 TERM 1 ENTRY EXAMS

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

1. Hii ni insha ya tawasifu
 - a. Lazima insha iwe na kichwa
 - b. Insha iandikwe katika nafsi ya kwanza umoja na kwa lugha nathari
 - c. Mtahiniwa aandike juu ya maisha yake tangu utotoni hadi wakati uliopo
 - d. Insha iwe na mpangilio mzuri kimantiki

Baadhi ya hoja

-Majina yake

-Tarehe na mahali pa kuzaliwa.

-Maisha ya utotoni (kabla ya kuingia shule)

-Maisha katika shule ya msingi

-Maisha katika shule ya sekondari

Tazama: Mtahini akadirie hoja za mtahiniwa

2. Vijana hujihusisha na visa vingi vinavyo onyesha utovu wa maadili. mifano, ulevi, matumizi ya dawa za kulevya, ngono, uavyaji mimba, lugha chafu, wizi, kupigana n.k

-Mtahiniwa apendekeze njia za kukabiliana na uozo huo.

Baadhi ya hoja

-Vijana wapewe ushauri nasaha

-Wajihusishe na michezo

-Wapewe mafunzo ya dini

-Nafasi za ajira ziongezwe

-Wazazi wawajibike katika malezi ya wanawe

-Wazazi wawe mfano bora kwa vijana

Taz. Mtahini akadirie hoja za mtahiniwa

3. Hii ni insha ya methali

-Maana ya methali; Mtu asiyetaka mwanawe alie huishia kulia yeye mwenyewe

-Methali hii huwanasihia wazazi wasichelee kuwadhibu watoto wao wanapokosea ili waishie kuwa na tabia na mienendo mizuri.

-Mtahiniwa atunge kisa ambacho kinalenga maana ya methali

-Mtahiniwa anaweza kueleza maana ya methali-si lazima

-Kisa kishughulikie pande zote mbili za methali.

4. Hii ni insha ya mdokezo

-Lazima insha ikamilike kwa mdokezo

TAZAMA: kwa viwango mbalimbali vya utuzaji tafadhali rejelea mwongozo wa kusahihisha mtihani wa pamoja wa kaunti ndogo ya Kirinyaga ya kati -2019